



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



23 Disemba, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UCHAGUZI WA VIONGOZI WA SHIRIKISHO LA NGUMI ZA WAZI TANZANIA (OBFT)

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT) kuwa, Uchaguzi wa viongozi wa Shirikisho hilo unatarajiwa kufanyika tarehe 12 Februari, 2023 Jijini Dar es Salaam.

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi tofauti za uongozi unatarajiwa kufanyika tarehe 10 Februari, 2023.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitaanza kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Mkapa na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz kuanzia tarehe 09/01/2022 hadi tarehe 07/02/2023.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

Nafasi	Ada
1. Rais	300,000/=
2. Makamu Rais	
3. Katibu Mkuu	
4. Katibu 200,000/=	Msaidizi
5. Mweka Hazina	
6. Mjumbe wa Kamati ya Walimu	
7. Mjumbe wa Kamati ya Waamuzi na Majaji	
8. Mjumbe wa Kamati ya Ufundi	
9. Mjumbe wa Kamati ya Mashindano na Vifaa	
10. Mjumbe Kamati Wanawake na 100,000/=	Vijana
11. Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Mikoa na Taasisi za Umma	

12. Mjumbe wa Kamati ya Mipango na Fedha
13. Mjumbe wa Kamati ya Afya
14. Mjumbe wa Kamati ya AOB, APB na WSB

Sifa za wagombea

1. Nafasi ya Rais hadi kwa Katibu Mkuu Msaidizi;

- i. Awe Raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- ii. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha 4 na kuendelea;
- iii. Awe amewahi kuongoza chama au taasisi yoyote ya umma au binafsi;
- iv. Rais awe na uzoefu wa uongozi kwa muda au kipindi kisichopungua miaka miwili;
- v. Makamu Rais awe hajawahi kuliongoza Shirikisho kwa awamu mbili mfululizo (yaani miaka minane mfululizo) katika moja ya nafasi zilizopo katika kundi la sekretarieti;
- vi. Awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai katika mahakama yoyote Tanzania;
- vii. Awe amethibitishwa na kamati ya Uchaguzi wa OBFT;
- viii. Awe na ujuzi wa mchezo huu katika Nyanja ya ualimu, uamuzi, uongozi na usimamizi wa mchezo wa ngumi za wazi;
- ix. Awe hajawahi kucheza, kuongoza au kuratibu mchezo wa ngumi za kulipwa katika ngazi yoyote;
- x. Awa ameisoma na kuilewa katiba ya OBFT na kuwa tayari kuilinda na kuitii.
- xi. Nafasi ya Katibu Mkuu na Makamu wake lazima wawe na elimu ya kutumia kompyuta katika matumizi ya kawaida na uzoefu wa uongozi.

Mweka hazina;

- i. Awe na sifa zote zilizotajwa katika nafasi za juu;
- ii. Awe na elimu ya uhasibu kuanzia ngazi ya cheti na kuendelea.

3. Sifa Wajumbe;

- i. Awe Raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- ii. Awe na ueledi wa kujua kusoma na kuandika;

- iii. Awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai katika mahakama yoyote Tanzania;
- iv. Awe hajaongoza shirikisho katika nafasi ya zote za juu;
- v. **Ni lazima mgombea wa nafasi ya ujumbe** awe amewahi kuucheza mchezo huu katika kipindi kisichopungua miaka mitano (5) mfululizo isipokuwa kwa mjumbe wa kamati ya wanawake mgombea sio lazima awe amewahi kuucheza mchezo huu.
- vi. Awe anazijua sheria za mchezo wa ngumi za ridhaa;
- vii. Awe hajawahi kucheza, kuongoza au kuratibu mchezo wa ngumi za kulipwa katika ngazi yoyote;
- viii. **Kwa kamati ya walimu mgombea** ni lazima awe na cheti cha ualimu wa mchezo wa ngumi katika ngazi yoyote;
- ix. **Kwa kamati ya afya na madaktari** mgombea lazima awe na taaluma ya udaktari wa michezo;
- x. **Kwa kamati ya wanawake** mgombea ni lazima awe ni mwanamke, awe amewahi kuongoza chama au taasisi yoyote ya umma na awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea;
- xi. Awa ameisoma na kuilewa katiba ya OBFT na kuwa tayari kuilinda na kuitii.

Malipo ya fomu yafanyike katika akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo Serikalini. Ili kupata namba ya utambulisho wa malipo (**control number**) mgombea atapiga namba za simu kwa namba, 0735 414 043 au 0735 892 889 kwa maelekezo zaidi.

Aidha, risiti ya malipo iwasilishwe Baraza pamoja na fomu zilizojazwa kwa usahihi na kuambatanishwa na nakala za nyaraka zote kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya OBFT.

Baraza linatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya mchezo wa ngumi za ridhaa nchini.

Imetolewa Na:



Najaha Bakari

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano.